

**REF: PPR/12 - 1/01**

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA MAFUTA AINA YA PETROLI KUANZIA  
JUMATANO, TAREHE 4 JANUARI 2012**

Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini katika mfumo wa uagizaji wa mafuta wa pamoja. Bei hizi zitaanza kutumika kuanzia **Jumatano, Tarehe 4 Januari 2012**. Pamoja na kutambua bei kikomo za bidhaa mbalimbali za petroli nchi nzima, ni muhimu kuzingatia yafuatayo.

- (a) Bei za jumla na rejareja kwa aina zote za mafuta zimebadilika ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 19 Desemba 2011. Katika toleo hili, bei za rejareja kwa aina zote za mafuta zimepanda kama ifuatavyo: Petroli imepanda kwa TZS 73.92/lita sawa na asilimia 3.93; Dizeli imepanda kwa TZS 1.04/lita, sawa na asilimia 0.05 na Mafuta ya taa yamepanda kwa TZS 4.59/lita, sawa na asilimia 0.23. Mabadiliko haya ya bei za mafuta hapa nchini yametokana na mabadiliko ya bei katika soko la dunia. Bei za jumla kwa kulinganisha matoleo haya mawili zimebadilika kama ifuatavyo: Petroli imepanda kwa TZS 67.24/lita sawa na asilimia 3.71, Dizeli imeshuka kwa TZS 1.04/lita, sawa na asilimia 0.05 na bei ya Mafuta ya Taa imeshuka kwa TZS 2.02/lita, sawa na asilimia (0.11).
- (b) Kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta ya mwaka 2008, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuzi ya bidhaa za mafuta.
- (c) **Kampuni za mafuta zipo huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani ilimradi bei hizo ziko chini ya bei kikomo (price cap)** kama ilivyokotolewa na *fomula* mpya iliyopitishwa na EWURA na ambayo ilichapwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 454 la tarehe 23 Desemba 2011.
- (d) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionyesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta kutoka kwenye vituo vinavyouza mafuta kwa bei ndogo zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja na adhabu itatolewa kwa kituo husika.**
- (e) Wanunuzi wanashauriwa kuhakikisha kuwa wanapata stakabadhi ya malipo inayoonesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hiyo ya malipo itatumika kama kidhibiti cha mnunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya ama kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo; ama endapo utakuwa umeuziwa mafuta yenye kiwango cha ubora kisichofaa.

## A: BEI ZA REJAREJA

Mji	Bei Kikomo		
	Petroli (TZS/LT)	Dizeli (TZS/LT)	Mafuta ya Taa (TZS/LT)
<b>Dar es Salaam</b>	1,956	1,977	1,963
<b>Arusha</b>	2,040	2,061	2,047
Arumeru (Usa West)	2,040	2,061	2,047
Karatu	2,058	2,079	2,065
Monduli	2,045	2,066	2,052
Ngorongoro (Loliondo)	2,096	2,117	2,103
<b>Kibaha</b>	1,960	1,982	1,967
Bagamoyo	1,967	1,988	1,974
Kisarawe	1,963	1,984	1,970
Mkuranga	1,966	1,987	1,972
Rufiji	1,983	2,005	1,990
<b>Dodoma</b>	2,015	2,036	2,021
Kondoa	2,047	2,068	2,054
Kongwa	2,012	2,033	2,018
Mpwapwa	2,016	2,037	2,022
<b>Iringa</b>	2,020	2,041	2,027
Kilolo	2,024	2,045	2,031
Ludewa	2,086	2,107	2,093
Makete	2,079	2,100	2,086
Mufindi (Mafinga)	2,030	2,051	2,036
Njombe	2,048	2,069	2,055
<b>Bukoba</b>	2,171	2,192	2,178
Biharamulo	2,145	2,166	2,152
Chato	2,128	2,149	2,135
Karagwe (Kayanga)	2,187	2,208	2,194
Muleba	2,171	2,192	2,178
Ngara	2,136	2,157	2,143
Misenyi	2,179	2,200	2,186
<b>Kigoma</b>	2,187	2,208	2,193
Kasulu	2,173	2,194	2,179
Kibondo	2,151	2,172	2,158
<b>Moshi</b>	2,029	2,051	2,036
Hai (Bomang'ombe)	2,033	2,054	2,039
Mwanga	2,023	2,044	2,029
Rombo (Mkuu)	2,050	2,072	2,057
Same	2,016	2,037	2,023
Siha (Sanya Juu)	2,036	2,057	2,043

<b>Lindi</b>	2,015	2,036	2,021
Kilwa Masoko	1,990	2,011	1,996
Liwale	2,036	2,057	2,042
Nachingwea	2,044	2,065	2,050
Ruangwa	2,042	2,063	2,049
<b>Babati</b>	2,078	2,099	2,085
Hanang (Katesh)	2,089	2,110	2,095
Kiteto (Kibaya)	2,089	2,110	2,096
Mbulu	2,091	2,112	2,097
Simanjiro (Orkasumet)	2,110	2,131	2,117
<b>Musoma</b>	2,134	2,155	2,141
Bunda	2,125	2,146	2,132
Serengeti (Mugumu)	2,180	2,201	2,186
Tarime	2,145	2,166	2,152
<b>Mbeya</b>	2,063	2,084	2,069
Chunya	2,072	2,093	2,079
Ileje	2,076	2,097	2,083
Kyela	2,079	2,100	2,085
Mbarali (Rujewa)	2,047	2,068	2,054
Mbozi (Vwawa)	2,072	2,093	2,079
Rungwe (Tukuyu)	2,072	2,093	2,078
<b>Morogoro</b>	1,981	2,002	1,988
Mikumi	1,996	2,018	2,003
Kilombero	2,019	2,040	2,025
Mahenge	2,029	2,050	2,036
Kilosa	1,999	2,020	2,006
Mvomero	1,991	2,012	1,998
<b>Mtwara</b>	2,028	2,049	2,035
Masasi	2,054	2,075	2,060
Newala	2,060	2,081	2,067
Tandahimba	2,053	2,074	2,060
<b>Mwanza</b>	2,106	2,127	2,112
Geita	2,147	2,168	2,153
Kwimba	2,142	2,163	2,148
Magu	2,114	2,135	2,120
Misungwi	2,111	2,132	2,118
Sengerema	2,138	2,159	2,145
Ukerewe	2,165	2,186	2,172
<b>Sumbawanga</b>	2,128	2,150	2,135
Mpanda	2,163	2,184	2,170
Nkasi	2,142	2,163	2,148
<b>Songea</b>	2,079	2,100	2,086
Mbinga	2,113	2,134	2,119
Namtumbo	2,108	2,129	2,115
Tunduru	2,138	2,159	2,145

<b>Shinyanga</b>	2,084	2,106	2,091
Kahama	2,098	2,119	2,105
Bukombe	2,110	2,131	2,117
Bariadi	2,126	2,147	2,132
Kishapu	2,113	2,134	2,119
Maswa	2,117	2,138	2,124
Meatu	2,124	2,145	2,131
<b>Singida</b>	2,046	2,068	2,053
Iramba	2,058	2,080	2,065
Manyoni	2,031	2,052	2,038
<b>Tabora</b>	2,110	2,131	2,116
Igunga	2,064	2,085	2,070
Nzega	2,074	2,095	2,081
Sikonge	2,122	2,143	2,128
Urambo	2,123	2,144	2,130
<b>Tanga</b>	2,002	2,023	2,009
Handeni	1,981	2,003	1,988
Kilindi	2,016	2,037	2,023
Korogwe	1,995	2,016	2,002
Lushoto	2,005	2,026	2,011
Mkinga (Maramba)	2,016	2,037	2,023
Muheza	2,002	2,023	2,009
Pangani	2,009	2,030	2,015

**B: BEI ZA JUMLA**

<b>Bei za Jumla - DSM</b>	<b>Petroli</b>	<b>Dizeli</b>	<b>Mafuta ya Taa</b>
<b>Bei Kikomo</b>	<b>1,881.92</b>	<b>1,903.04</b>	<b>1,888.59</b>

**Haruna Masebu**  
**MKURUGENZI MTENDAJI**  
**EWURA**